

Utangulizi.

Kuna zaidi ya miti 50 ya matunda ya asili kati-ka Misitu ya Miombo nchini. Matunda haya yana utajiri wa sukari, madini, vitamini na viini muhimu kwa ajili ya tiba ya magonjwa ya binadamu na mifugo.

Umuhimu wake

Hivyo yanaweza kuwa chanzo muhimu sana cha chakula, lishe na madawa. Hivyo yanaweza kusaidia kupiga vita utapiamlo na upungufu wa vitamin A na C, amino asidi muhimu na madini kama chuma na zinki.

Matunda asili maarufu hasa mkoa wa Tabora na miko ajirani ni kama vile Ntalali, ntonga, mbula, mfuru, ukwaju, ubuyu na maembe.

Upatikanaji wake

Matunda ya asili yaliyo mengi hukomaa wakati wa kiangazi ambapo mara nyingi huwa kuna upungufu wa chakula. Hivyo matunda haya yanaweza kusaidia kuboresha lishe hasa vijijini.



Mti wa matunda ya asili aina ya mantonga uliopandwa kituoni TARI Tumbi

Ili kurahisisha upatikanaji wa matunda na madawa ya asili Kituo cha utafiti cha TARI Tumbi kwa kushirikiana na mashirika ya utafiti ya kimataifa kimegundua teknolojia ya upandaji wake.

Baadhi ya miti hii imepandwa katika mashamba ya utafiti kituoni. Miti iliyopandwa ni kama ntalali (*Vitex mombasae*), mantonga (*Strychnos cocculoides*) na Mbula (*Parinari curastellifolis*)

Upandaji wa miti ya matunda ya asili utaongeza upatikanaji wake na hifadhi, kupunguza uharibifu wa mazingira na kuongeza hifadhi ya vinasaba vya matunda haya.

Jamu iliyotengenezwa kutokana na matunda ya asili na baadhi ya vyakula



ambavyo vinaweza kutumiwa ili kuviongezea ladha

Uongezaji thamani

Halikadhalika Kituo hiki cha utafiti kimefanikiwa kuibua teknolojia ya usindikaji wa matunda ya asili kutengeneza bidhaa kama juisi, jamu na mvinyo.

Hii itasaidia kuongeza thamani matunda ya asili ambayo yalikuwa yanapewa thamani ndogo na jamii. Hivyo itaongeza upatikanaji wa lishe na pia kipato kwa wakulima. Pia itasaidia kuhifadhi mazingira na miti hii, kwani jamii itatambua thamani halisi kwa ustawi wake.

Kituo cha TARI Tumbi kimeshafundisha teknolojia hii kwa wakulima zaidi ya 3000 katika mkoa wa Tabora.

Licha ya kuongeza ulaji wa matunda ya asili, usindikaji huu utapunguza upotevu, utaongeza soko na utaongeza thamani ya matunda ya asili. Pia utaongeza kipato hasa kwa akina mama hivyo kupunguza kiwango cha umaskini hasa vijijini.

Baadhi bidhaa zinazoweza kutengenezwa kutokana na matunda ya asili ni jamu, juisi na mvinyo.

Jamu

Jamu ni aina ya chakula kinachotengenezwa kutokana na matunda ya asili. Hivyo kina vitamini kwa wingi. Jamu hupakwa ili kuongeza ladha vyakula kama mikate, maandazi, ndizi na viazi

Mama akinywa juisi iliyotengenezwa kutokana na matunda ya asili



Juisi

Juisi ni kinywaji baridi ambacho hutengenezwa kutokana na matunda ya asili na ina virutubisho vingi aina ya vitamin na madini. Kinywaji hiki hunywewa baada ya chakula au kabla ya chakula ili kuongeza hamu ya kula na kuongeza lishe ya mlaji

Mvinyo

Hiki ni aina ya kinywaji chenye kilevi. Hutengeneza kutokana na matunda mbalimbali ya asili kama zambarau, mantonga au mahama.. Mvinyo hunywewa kama kiburudisho baada ya masaa ya kazi.



Miti

ya tiba ya asili

Misitu ya Miombo in utajiri mkubwa wa miti ambayo imekuwa inatumiwa kwa ajili ya tiba ya wanadamu pamoja na mifugo. Kituo cha TARI Tumbi baada ya kufanya utafiti kimepanda baadhi ya miti hiyo kituoni kwa ajili ya utafiti zaidi, kuihifadhi pia kurahisisha upatikanaji wake.

Baadhi ya miti hiyo ni milundalunda na misana, mizima, mlungulungu na mnengo nengo. Baadhi ya miti ya madawa ya asii imepandwa kituoni TARI Tumbi kwa ajili ya utafiti zaidi.

Miti hii hutumika na waganga wa jadi katika kutoa tiba ya magonjwa ya binadamu na wanyama.

Miti ya madawa ya asili iliyopandwa kituoni Tumbi ni kama Mlundalunda (*Cassio abbreviate*), Mlungulungu (*Zanthoxylum chalybeum*), Mzima (*Terminalia sericea*) na Msana (*Combretum zeyheri*).

Baadhi ya magonjwa ya binadamu yanayotibiwa ni kama magonjwa ya tumbo, malaria, magonjwa ya ngozi, kichwa na matatizo ya uzazi.

Jaribio la miti ya madawa ya asili lililopandwa



kituoni TARI Tumbi

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania



KITUO CHA TUMBI TABORA



UPANDAJI WA MITI YA MATUNDA NA YA MADAWA YA ASILI

Kimeandaliwa na Kituo cha TARI –Tumbi

Mawasiliano:
Mkurugenzi wa Kituo
TARI Tumbi
S.L.P. 306
TABORA
Barua pepe: cdtumbi@tari.go.tz
Simu: +255 732 988885
Fax: +255 732 988848
Wavuti: www.tari.go.tz

Chapisho Na. 2019/6